

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**

Simu Na.  
Mkurugenzi Mezani: 027-2757101  
Simu ya Ofisi: 027-2757102  
Nukushi: 027-2758929  
Website:www.rombodc.go.tz



Kumb. Na: HWR/M20/1/VOLI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji  
S.L.P 52  
Mkuu-Rombo

04/11/2021

## **TANGAZO LA KUWATAFUTA MAFUNDI WA UJENZI KITUO CHA AFYA MKUU WILAYA YA ROMBO.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo amepokea Fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mkuu Wilaya ya Rombo itakayo jengwa katika Tarafa ya Mkuu kata ya Kelamfua Mokala.

Mkurugenzi Mtendaji anapenda kuwatangazia mafundi wote wa ujenzi (Local Fundi) wenye uwezo na sifa za kujenga majengo ya Serikali.

Halmashauri ya Wilaya ya Rombo inategemea kujenga na kukarabati majengo matano(5).

mafundi wenye uwezo wa kujenga watapewa fomu maalumu (schedule of Labour) ambazo zitapatikana katika ofisi ya Kitengo cha manunuzi kwa gharama ya Tsh 30,000/= kwa kila kabrasha ambazo hazitarejeshwa.

Baada ya kuzijaza hizo fomu za ujenzi wa wodi zitawasilisha kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Wilaya S.L.P 52 Rombo.

### **Sifa mwombaji:-**

- 1.Awe na picha za miradi aliyowahi kufanya zikimuonyesha akiwa anafanya kazi za ujenzi.
2. Awe raia wa Tanzania mwenye uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na pia awe na umri kuanzia miaka kumi na nane (18) na kuendelea.
- 3.Awe na uwezo wa kusimamia na kuwaongoza mafundi wasaidizi.

- 4.Awe na uelewa mzuri wa usalama na afya awapo eneo la kazi.
- 5.Awe na timu ya kutosha ya mafundi wasaidizi wa kada mbalimbali.
- 6.Awe na uwezo wa kuandaa na kuutekeleza mpango kazi wa mradi.

### **Uzoefu:-**

- 1.Uzoefu wa miaka mitano na kuendelea katika kufanya kazi za ujenzi.
- 2.Awe amefanya kazi yoyote ya serikali walau mradi mmoja.
- 3.Awe na uzoefu wa kusoma na kutafsiri michoro ya majengo.
- 4.Awe na uzoefu wa kutumia vifaa na teknolojia za kisasa za ujenzi.

Maombi yote yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa anuani ifuatayo:- **Katibu wa Bodi ya Zabuni S.L.P 52, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo**, mwisho wa kupokea maombi hayo ni saa 4:00 asubuhi siku ya Alhamis tarehe 11/11/2021.Sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Rombo utatumbukiza maombi hayo katika sanduku la zabuni(TENDA BOX).

Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo mbele ya waombaji watakaopendelea kuhuduria ufunguzi huo.

Tangazo limetolewa



Charles Mganga

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (H/W)**  
**ROMBO.**

